

KIZIDUO
MUHTASARI WA KIKAO CHA WAKUU WA IDARA NA VITENGO
(CMT) KILICHOFANYIKA UKUMBI MKUBWA WA JIJI TAREHE
22/10/2021.

WATENDAJI WALIOHUDHURIA

NA	JINA KAMILI	CHEO
1	Ndg. Julius Mulongo	Kaimu Mkurugenzi Jiji
2	Ndg. S. A. Kaunara	Afisa Utumishi Mkuu Jiji
3	Ndg. Maliki A. Mweneyuni	Kaimu Mwanasheria Jiji
4	Ndg. Neema Mallya	Kaimu Mweka Hazina Jiji
5	Ndg. Walyama S. Tundosa	Mchumi wa Jiji
6	Ndg. Godbless urio	Mkaguzi wa Ndani Jiji
7	Ndg. Costansia Gabusa	Afisa Maendeleo ya Jamii Jiji
8	Ndg. Deogratias Justus	Afisa Nyuki Jiji
9	Ndg. Venance M. Joseph	Kaimu CPO
10	Ndg. Martin M. Sawema	Afisa Habari
11	Ndg. Hosiana Kusiga	Kaimu Afisa Mipango Miji Jiji
12	Ndg. Salome L. Nzingula	Kaimu Afisa Kilimo, Umwagiliaji & Ushirika Jiji
13	Ndg. Desdenus M. Polle	Kaimu Afisa Mazingira Jiji
14	Ndg. Eveline R. Ntahamba	Mhasibu Matumizi
15	Ndg. Venance Babukege	Afisa Elimu Sekondari Jiji
16	Ndg. Nyandaro Msagasa	Kaimu Afisa Elimu Msingi Jiji
17	Ndg. Japhari S. Kasusura	Mratibu – TASAF
18	Eng. Tunaye N. Mahenge	Kaimu Mhandisi Jiji

SEKRETARIETI

NA	JINA KAMILI	CHEO
1	Ndg. Dickson Johnson M.	Mwandishi wa Vikao
2	Ndg. Joshua Nyasi	Mwandishi wa Vikao

AGENDA ZA KIKAO.

1. Kufungua kikao.
2. Ombi la kuidhinisha kupunguza ada ya shule ya Nyanza English Medium School toka Tshs. 600,000.00 hadi Tshs. 400,000.00.
3. Ombi la idhini ya kulipa deni la Tshs. 13,209,330.50 kwa Mkandarasi M/S DITCHET CO.LTD.
4. Taarifa ya kusudio la ujenzi wa bwawa la kuchujia maji taka maegesho ya magari, njia za kuzunguka jengo na kutengeneza mazingira yanayozunguka jengo la wodi ya Wanaume Nyamagana Hospitali.
5. Taarifa ya hatua iliyofikiwa katika miradi ya maendeleo ya kuongeza mapato iliyopelekewa fedha.
6. Taarifa ya mapokezi ya fedha za UVIKO-19 kwa ajili ya kujenga vyumba vya madarasa 98 shule za Sekondari kiasi cha **Tshs. 1,960,000,000.00**
7. Kufunga kikao

AGENDA NA. 24/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO.

Mwenyekiti alifungua kikao saa 01:55 asubuhi kwa kuwakaribisha Wajumbe kwenye kikao.

AGENDA NA. 25/2021/2022: KUTHIBITISHA AGENDA.

Wajumbe walithibitisha agenda zote na kisha kuridhia zija diliwe katika kikao.

AGENDA NA. 29/2021/2022: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA UVIKO-19 KWA AJILI YA KUJENGA VYUMBA VYA MADARASA 98 SHULE ZA SEKONDARI KIASI CHA TSHS. 1,960,000,000.00

Afisa Mipango, Takwimu na Ufuatiaji kwa niaba ya Mkurugenzi aliwasilisha taarifa ya Mapokezi ya fedha za UVIKO 19 katika shule mbalimbali za Halmashauri ya Jiji la Mwanza na kueleza kuwa Fedha zilizotolewa ni kiasi cha shilingi 1,960,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Madarasa 98 na kueleza changamoto ambazo zimejitokeza kuwa ni baadhi ya maeneo kupelekewa fedha hizi ili hali wakiwa hawana eneo la kujenga na kutolea mfano shule ya sekondari butimba na Mwanza sekondari.

Wajumbe walipokea na kabla ya kuridhia walimpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ndg Samia Suluhu Hassan na kuomba ufafanuzi juu ya maelekezo yaliyotolewa kuhusiana na ujenzi wa madarasa yake. Afisa mipango alieleza kuwa maelekezo ni kwamba madarasa hayo yanatakiwa kukamilika kabla ya Tarehe 30/12/2021 na ujenzi wake unatakiwa kujenga kwa kutumia force akaunti.

Wajumbe walishauri kutokana na uhaba wa maeneo katika maeneo mengi ni vyema ikafanyika tathimini katika maeneo ambayo yana nafasi yakajengwa madarasa ya kawaida na kushauri kuona namna Halmashauri inavyoweza kutoa fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa kwa mwaka 2021/2022 zikaongezwa ili kujenga madarasa kwa njia ya ghorofa katika maeneo ambayo hayana nafasi.

Afisa mipango alipokea ushauri huo na kuahidi kushirikiana na afisa Elimu sekondari ili kuweza kufanya tathimini ni maeneo yapi yanaweza kujengwa